**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO**
**SHULE YA SEKONDARI KWEMARAMBA**
**S.L.P 1O3, LUSHOTO**

**Website** [www.sites.google.com./Site/kwemarambass/home](www.sites.google.com./Site/kwemarambass/home)
**Tel: 0658819057/0684000791 (Mkuu wa Shule),KUMB. Na KMSS/C/PS/V.3/2026/31**

**Jina la Mwanafunzi**…………………………………………

**<u>FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO…………..KATIKA SHULE YA SEKONDARI KWEMARAMBA.</u>**

**SEHEMU A: UTANGULIZI**

1. Hongera sana kwa kuchaguliwa kujiunga na **Kidato cha Tano** mwaka……………katika shule ya sekondari Kwemaramba, tahasusi ya ………
2. Ukiwa Kwemaramba sekondari, utalazimika kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za shule kwa ajili ya mafanikio yako kitaaluma na kijamii.
3. Utaripoti shuleni tarehe…………………..bila kuchelewa. Hata hivyo, kama serikali itatangaza tarehe nyingine tofauti na hii, utatakiwa kuripoti kwa kuzingatia tarehe ya Serikali.

**<u>SEHEMU B: MAHALI SHULE ILIPO NA JINSI YA KUFIKA SHULENI</u>**

Shule ipo mkoa wa **Tanga, Wilaya ya Lushoto, Tarafa ya Mlalo kata ya Dule M** karibu na Mji mdogo wa **Moa.** Kuna mabasi ya moja kwa moja kutoka katika miji ya Dar-es –salaam, Arusha,Dodoma na Tanga yanayokwenda Lushoto – Mlalo. Ukipanda gari ya kuja Lushoto - Mlalo telemka katika kituo kinachoitwa **MAJULAI** kisha panda bodaboda kwa shilingi **2,500/=** TU hadi shuleni. Kama utapanda basi linaloishia Lushoto mjini kuna usafiri wa mabasi au **NoaH** na nauli ni shilingi **6,000/=** TU mpaka **MAJULAI.** Ukifika shuleni ripoti moja kwa moja kwa **OFISI YA MKUU WA SHULE.**
Baada ya kuripoti taratibu nyingine zitafuata.

***<u>SEHEMU C: SARE YA SHULE NA MAHITAJI MENGINE MUHIMU – KWA WAVULANA.</u>***

| Na. | SARE/MAHITAJI | MAELEZO |
|---|---|---|
| 1 | Suluari mbili (2) nyeusi za darasani zisizobana,zisizo na marinda na zenye mfuko mmoja wa nyuma na isiwe modo , iweze kuvuka goti bila kubana ikipandishwa juu. | Ashoneshe popote |
| 2 | Mashati mawili (2) ya tetron spesho rangi nyeupe mikono mirefu | Anunue popote |
| 3 | Tai nyeusi kwa ajili ya kuvaa darasani | Ashoneshe popote |
| 4 | Tracksuit rangi ya **dark blue** kwaajili ya michezo. | Unaweza kuzipata duka la shule kwa gharama ya tsh 25,000/= ukipenda |
| 5 | Boshori la kuvaa kichwani wakati wa usiku(prepo) rangi ya **bendera ya taifa. NB. Isiwe na chata yoyote.** | Anunue popote |
| 6 | Mkanda wa suluari wa kawaida rangi nyeusi | Anunue popote |
| 7 | Socks rangi nyeusi jozi mbili (2) au Zaidi | Anunue popote |
| 8 | Masweta mawili (2) rangi ni kijani cheusi. | Unaweza kuipata duka la shule kwa bei ya shilingi 25,000/=Sweta moja. |
| 9 | T- shirt mbili zenye rangi ya moja kijani na nyingine blue kwa ajili kushindia na kuvaa kwenye matukio maalumu. | Unaweza zipata shuleni kwa bei ya Shilingi 25,000/=T-shirt moja ukipenda. |
| 10 | Kaunda suti jozi mbili za kushindia suluari na shati lenye kola, mikono mirefu rangi ni **DAMU YA MZEE**(Akiripoti awe amevaa) | Anunue/ashoneshe popote |
| 11 | Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vya kufunga na kamba (visiwe buti au vyenye visigino virefu) | Anunue popote |
| 12 | Shuka mbili (2) za rangi ya **BLUE BAHARI.** | Anunue popote |
| 13 | Vifaa vya chakula ikiwa ni pamoja na sahani, kikombe na bakuli za shaba au aluminiamu na kijiko | Anunue popote |
| 14 | Picha mbili (2) za Passport size | Apige popote |
| 15 | Chandarua kimoja (1) | Anunue popote |
| | GODORO. | KWA ANAYETAKA LINAPATIKANA SHULENI KWA TSH. 10,000/= KWA MUHULA MMOJA. |
| | Sanduku imara la bati (tranka) kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyake | Anunue popote |

| | | |
|---|---|---|
| 18 | **Vifaa vya usafi shuleni** ( ufagio wa nje wa kusimama, brashi ngumu ya kusugulia sakafu na brashi ngumu ndogo ya kusugulia sinki la choo, mopa laini ya kukaushia sakafu, na mopa ngumu ya kusafishia sakafu bwenini na darasani.,panga na jembe kwa ajili shughuli mbalimbali za kazi.)<br><br>N.B,Aje na ndoo mbili (02) ndogo kwa ajili ya maji ya kunywa na usafi wake binafsi. | Vifaa hivi vinapatikana kwenye DUKA la shule kwa gharama ya Shilingi, 35,000/= TU. |
| 19 | Aje na **Bima ya Afya** kama hana anapaswa kuwa na fedha ya akiba itakayokusaidia katika matibabu hapa shuleni.<br>N.B. **shule inatoa huduma ya kwanza TU.** | Uje na shilingi **15,000/=** kwa ajili huduma ya kwanza hapa shuleni. |

**SEHEMU D: SARE YA SHULE NA MAHITAJI MENGINE – WASICHANA**

| Na. | SARE/MAHITAJI | MAELEZO |
|---|---|---|
| 1 | Sketi mbili (2) nyeusi za darasani ziwe ndefu na kufika karibu na kifundo cha mguu na hijabu nyeupe ya kushona na isiwe na urembo na iwe ya heshima kwa waislamu (nusu kanzu na suluari haviruhusiwi) | Ashoneshe popote |
| 2 | Mashati mawili (2) ya tetron spesho rangi nyeupe mikono mirefu | Anunue popote |
| 3 | Neck tie mbili (2) nyeusi kwa ajili ya kuvaa Darasani | Ashoneshe popote |
| 4 | Tracksuit rangi ya dark blue kwa ajili ya michezo. | Unaweza ukazipata Shule kwa tsh 25,000 kama utapenda. |
| 5 | Boshori la kuvaa kichwani wakati wa usiku (prepo) rangi ya **bendera ya taifa**. | Anunue popote |
| 6 | Socks rangi nyeupe jozi mbili (4) au zaidi | Anunue popote |
| 7 | Masweta mawili (2) rangi ni kijani cheusi. | Unaweza ukaipata kwenye duka la shule kwa bei ya shilingi 25,000/=TU ukipenda. |
| 8 | T- shirt mbili rangi ya kijani na blue,kwa ajili ya kushindia na kuvaa kwenye matukio maalumu. | Unweza ukaipata kwenye duka la shule ukipenda kuinunua shuleni kwa bei ya Shilingi 25,000/=kwa kila moja. |
| 9 | Gauni mbili za kushindia kitambaa na mshono wa kawaida (Shamba dress) rangi ya damu ya mzee aje akiwa amevaa moja | Anunue/ashoneshe popote |
| 10 | Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vya kufunga na kamba (visiwe buti au vyenye visigino virefu) | Anunue popote |
| 11 | Shuka mbili (2) za rangi ya blue bahari | Anunue popote |

| | | |
|---|---|---|
| 12 | Vifaa vya chakula ikiwa ni pamoja na sahani, kikombe na bakuli za shaba au aluminiamu na kijiko. | Anunue popote |
| 13 | Picha mbili (2) za Pasport size | Apige popote |
| 14 | Chandarua moja (1) | Anunue popote |
| 15 | GODORO | KWA ANAYETAKA LINAPATIKANA SHULENI KWA 10,000/= KWA MUHULA |
| 16 | Sanduku imara la bati (tranka) kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyake | Anunue popote |
| 17 | **Vifaa vya usafi** ( ufagio wa nje wa kusimama, brashi ngumu ya kusugulia sakafu wa kusimama na brashi ngumu ndogo ya kusugulia sinki la choo, mopa laini ya kukaushia sakafu na mopa ngumu ya kusafishia sakafu bwenini na darasani.panga na jembe kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kazi.<br><br>**N.B,**Aje na ndoo mbili ndogo kwa ajili ya maji ya kunywa na usafi wake binafsi. | Vifaa vyote hivyo vilivyotajwa hapo vinapatikana shuleni kwa gharama ya shilngi **35,000/=** |
| 18 | Aje na Bima ya Afya kama hana anapaswa kuwa na fedha ya akiba itakayomsaidia katika matibabu hapa shuleni.<br>**N.B.shule inatoa huduma ya kwanza TU**. | Uje na kadi ya bima ya afya kama hauna, shule inautaratibu wa huduma ya afya. |

**SEHEMU E: VIFAA VYA DARASANI – KWA WOTE.**

1. Ufike na daftari za kutosha (kuanzia Counter book 12, Quire 3 au 4) kwa ajili ya masomo yako, kalamu, penseli na mkebe (Mathematical Set)
2. Kikokotoo cha sayansi na Hisabati (Scientific Calculator) na calculator hiyo iwe "**non-programmable calculator"** (Kama una wasiwasi wa kuuziwa feki njoo na pesa utapata shuleni).
3. Spring file mbili (2) za plastic
4. Kwa tahasusi za PCM na PCB awe na koti la maabara ( **LAB KOTI**) lenye **NEMBO** ya shule kwa ajili mazoezi kwa vitendo yanapatikana kwenye duka la shule (fundi wa shule) **kwa shilingi 35,000/=TU.**
5. Kwa wale wa PCB awe na **Dissecting kit** moja (1)zinapatikana shuleni Tsh 20,000/=
6. Kila mwanafunzi aje na rimu moja **Size A4 (AINA YA RIMU A-ONE)** kwa kila robo muhula wa masomo.

**N.B,Rimu zinapatikana kwenye duka la shule.**

**SEHEMU F: MICHANGO MUHIMU YA SHULE – KWA WOTE.**

**(LIPA KWENYE AKAUNTI YA NMB NAMBA 41603500041 YENYE JINA KWEMARAMBA SECONDARY SCHOOL**

| | MICHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Kitambulisho cha mwanafunzi (SCHOOL ID) | 5,000/= |
| 3 | Tahadhari (hairudishwi) | 5,000/= |
| 5 | Nembo ya shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | 80,000/ |

**MUHIMU**

1. Mwanafunzi aje na risiti ya malipo ya benki (bank pay in slip –**BPS)**
2. Mwanafunzi atapokelewa tu iwapo amekamilisha kulipa michango na kukabidhi vifaa vyote vilivyoagizwa.
3. Mwanafunzi anashauriwa awe na fedha za mfukoni (pocket money) kwa matumizi binafsi.
4. Hakikisha unasoma kwa makini maelekezo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Kama kuna sehemu hujaelewa uliza kwa uongozi wa shule baada ya kuripoti.
5. Kuhusu vitabu vya kununua mwanafunzi ataelekezwa na walimu husika atakapofika shuleni.

**Karibu kwemaramba sekondari.**

**…………………………**

**AMIRI J SHEHOZA**
**MKUU WA SHULE**

**0658819057/**
**0684000791**

KIAMBATISHO A

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI KWEMARAMBA, S.L.P 103, LUSHOTO**
**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

## 1. NIDHAMU

(a) Mwanafunzi atasimama kumsalimia mwalimu au mtu yoyote aliyemzidi umri anapopita au anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.

(b) Mwanafunzi atatumia lugha safi (inayokubalika) wakati wote anapowasiliana na wenzake na kwa watu wengine akiwa ndani au nje ya shule

(c) Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote na watu wengine

(d) Mwanafunzi ataitika wito mara moja pindi atakapoitwa.

(e) Mwanafunzi anapaswa kuheshimu kazi yoyote anayopewa na mwalimu au mlezi wake

(f) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na alama zingine za Taifa.

(g) Mwanafunzi atasimama katika mstari wakati wote anaposubiri kupata huduma

(h) Mwanafunzi atakaa kimya wakati wote akiwa darasani, asitoke nje ya darasa au eneo la shule bila ruhusa ya mwalimu

(i) Mwanafunzi anatakiwa kuwa mvumilivu kwa mambo yasiyo athiri utu wake katika mambo mbalimbali anayokumbana nayo shuleni au nje ya shule

(j) Mwanafunzi anatakiwa kutii walimu, watumishi wasio walimu, viranja na wanafunzi wenzake

(k) Mwanafunzi anatakiwa kutunza na kuthamini muda

(l) Mwanafunzi anatakiwa kuwa na ushirikiano ili apate mafanikio ya kielimu

## 2. MAHUDHURIO

**(a)** Mwanafunzi anatakiwa ahudhurie vipindi vyote vya darasani kwa muda wote wa masomo. Atatakiwa kufika shuleni kwa tarehe zote zilizopangwa na kama atafika kwa kuchelewa siku atakaporipoti akatoe taarifa kwa wafuatao

(i) Mwalimu wa zamu wa siku hiyo
(ii) Mwalimu wa darasa
(iii) Makamu wa mkuu wa shule
(iv) Walezi wa bweni.

(b) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano ya shule kama vile mabaraza ya shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya taifa na “roll call”

(c) Mwanafunzi atatakiwa kuwahi katika shughuli zote shuleni kama zilivyopangwa kwenye ratiba ya shule na pia anatakiwa kuwahi anapotakiwa au anaposikia kengele

(d) Mwanafunzi atatakiwa kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote anayopewa na mwalimu wa somo darasani. Akikosa jaribio au mtihani wowote akamuone mwalimu wa somo na mwandamizi taaluma.

(e) Mwanafunzi anatakiwa kutii mara moja wito wadharura

## 3. SARE YA SHULE NA MAVAZI

Mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare safi ya shule wakati wote wa saa za masomo. Atakuwa na vazi tofauti pale tu atakapoagizwa kama vile nguo za michezo wakati wa michezo au nguo za kushindia. Shule yetu ina utaratibu wa wanafunzi wote kuwa na mavazi ya nje ya madarasa yaani "**shamba dress".** Hivyo **hairuhusiwi** kabisa kwa mwanafunzi kuja shuleni na mavazi mengine ambayo siyo sare na yasiyoruhusiwa shuleni. Ikiwa mwanao atakuja shuleni na mavazi zaidi ya yale yaliyoruhusiwa, atataifishwa na hatarudishiwa kamwe bali yatateketezwa. Hivyo mzazi, mtoto wako anapofungasha sanduku lake **mkague** kwa umakini mkubwa TAFADHALI.

## 4. MAKATAZO

### 4.1 SEHEMU ASIZORUHUSIWA KUTEMBELEA MWANAFUNZI

**(a)** Mwanafunzi asitembelee sehemu zifuatazo isipokuwa kwa ruhusa

i. Ofisi ya walimu
ii. Maabara
iii. Nyumba za walimu na wafanyakazi
iv. Chumba cha walimu au wafanyakazi

**(b)** Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutembelea sehemu hizi:

i Vilabu vya pombe
ii. Kumbi za starehe
iii. Nyumba za kulala wageni
iv. Ndugu bila ruhusa

**(c)** Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa/kibali maalum.

**(d)** Mwanafunzi hatakiwi kuonekana bwenini wakati wa darasani bila kibali cha matron au patron au mwalimu wa zamu

**(e)** Muda wa kusoma usiku (night preparation) ni kuanzia saa 1:OO Kamili usiku hadi saa 4:00 usiku na baada ya hapo taa zote zitazimwa madarasani na unapaswa kurejea mara moja kitandani kwako.

### 4.2 NI MARUFUKU

(a) Kuiba mali ya mtu binafsi au umma
(b) Kufanya uasherati, ubakaji, usagaji au ushoga
(c) Kulewa kilevi cha aina yoyote, kuvuta sigara au bangi
(d) Kupiga au kupigana
(e) Kuharibu mali ya umma
(f) Kuoa au kuolewa
(g) Kutukana
(h) Kumiliki simu, laini ya simu, chaja ya simu, vocha ya simu na (kifaa kingine chochote cha simu), kamera, redio na pasi shuleni. Iwapo mwanafunzi atapatikana na vitu hivyo shuleni vitachukuliwa na havitarudishwa kamwe na mwanafunzi atafukuzwa shule. Ili kuepuka adha hiyo hakikisha kuwa humpi mwanao vitu hivyo visivyokubalika shuleni. Ili kurahisisha mawasiliano, unaweza kumwandikia mwanao namba ya simu ambayo ataitumia akihitaji mawasiliano na mzazi au mlezi na atasaidiwa mawasiliano ya simu na ofisi ya mkuu wa shule kupitia namba zilizoorodheshwa hapo juu.

**5. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE .**

(a) Uasherati, ubakaji, usagaji, ushoga, ulawiti, kuoa au kuolewa
(b) Wizi, ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
(c) Kuvuta bangi au sigara
(d) Kupiga au kupigana
(e) Kudharau bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya taifa, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(g) Kupata, kutoa, kushawishi kutoa au kusababisha mimba shuleni au nje ya shule
(h) Kugoma, kuongoza, kuchochea mgomo au vurugu, kuvuruga amani au usalama wa watu.
(i) Kukashifu na kukataa adhabu halali
(j) Kumiliki au kutumia simu shuleni au kumiliki kifaa chochote cha simu (kama chaja, vocha, headphone, laini nk..)
(k) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu nk.

**ANGALIZO**

Ni jukumu la mwanafunzi kufuata sheria na taratibu zilizowekwa ili kuepuka adhabu na kufukuzwa shule.

Walimu shuleni ni waelekezaji, walezi, waelimishaji na washauri. Mwanafunzi akiwasikiliza atafika kule anakotarajia, alikopanga. Aidha, shule ina utaratibu wa kumuita mzazi/mlezi shuleni pale ambapo mwanafunzi amepatikana na utovu wa nidhamu mkubwa hivyo ni vizuri kuwaasa watoto wenu kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za shule ili kuepuka usumbufu wa kuitwa shuleni.

**Jina…………………………………………………………………………saini…………………...**

**Tarehe……………………………………………**

**KIAMBATISHO B.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PMO-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**KWEMARAMBA SECONDARY SCHOOL,**
**P.O. BOX 103,**
**LUSHOTO.**
**Tarehe……………….**

**KMB. Na KMSS/C/PS/V.1/2023/08**
**TO MEDICAL OFFICER.**
**………………………………………**
**……………………………………….**

**REF: STUDENT MEDICAL EXAMINATION FORM.**

**Please Examine student named …………………………………………………….in respect of these areas and any other areas deemed relevant in connection to whether the student has problems related to**

**(a) Sight Yes/No. If yes,**
**state………………………………………………………………………………………**
**…………………………………………………………………………………………….**

**(b). Hearing Yes/No If yes,**
**state………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………………….**

**(c ). T.B. or any other chronic Diseases.Yes/No If yes,**
**state………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………………….**

**(d) Blood pressure. Yes/No If yes,**
**state………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………………….**
**…………………………………………………**

**(e) Any physical impairment(s).Yes/No If yes,**
**state………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………………….**

**Do you therefore recommend this pupil to pursuer studies at this school?.**
**……………………………………………………………………………………………….**
**……………………………………………………………………………………………….**

**Name……………………………………………………….**
**Signature……………………………………date………………**

**Official title…………………………………………Official stamp………………..**

**KIAMBATISHO C**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU– TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO**

**SHULE YA SEKONDARI KWEMARAMBA, S.L.P 103, LUSHOTO**

**KUMB. Na. KMSSS A. 1/K5/Vol.21**

**MZAZI/MLEZI WA ……………………………………………………………. …………**

**YAH: MAELEZO YA KUKUBALI NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI KWEMARAMBA MWAKA………………………..**

**Jaza panapohusika**

1. Mimi mzazi/mlezi wa …………………………………………………….......................
Nakubali/sikubali nafasi ya kujiunga na kidato cha Tano katika shule ya sekondari Kwemaramba…………………….kwasababu………………………………………………
…………. Naahidi nitatimiza/sitatimiza mahitaji yote muhimu kwa ajili ya kumwezesha mwanangu kuendelea na masomo katika kipindi chote atakachokuwa hapo shuleni. Aidha naahidi kuwa nitamshauri vizuri mwanangu hasahasa wakati wa likizo kuhusu mwenendo bora wa kitabia ili afanikiwe katika masomo na hatimaye kuwa raia mwema na mwenye ushirikiano na uzalendo.
2. Mimi mwanafunzi ……………………………………………………………………
ambaye nimechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Kwemaramba tahasusi ya ……..
nakubali/sikubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari Kwemaramba. **Naahidi nitatimiza na kufuata kanuni, taratibu na sheria zote zilizowekwa na shule na serikali ili niweze kuendelea na masomo kwa amani.**

   Jina langu……………………………………..Saini …………………… Tarehe……..

3. Maelezo haya yamethibitishwa/ yatathibitishwa na

……………………………………

AMIRI J SHEHOZA

MKUU WA SHULE

0658819057/0684000791.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI KWEMARAMBA**

**PICHA YA MWANAFUNZI**

JINA LA MWANAFUNZI……………………………………….MCHEPUO……………………FORM…………MWAKA……..

**PICHA NA NAMBA ZA SIMU ZA WAZAZI AU WALEZI,NDUGU WATAKAO WASILIANA NA MWANAFUNZI <u>AU KUFIKA SHULENI KUMUONA MWANAFUNZI</u>.**

1.

JINA………………………………………….

UHUSIANO NA MWANAFUNZI………………………….
NAMBA ZA SIMU ……………

2.

JINA………………………………………..

UHUSIANO NA MWANAFUNZI………..
NAMBA ZA SIMU ……………………..

3.

JINA……………………………………………………
UHUSIANO NA MWANAFUNZI…………….
NAMBA ZA SIMU…………………………….

4.

JINA…………………………………………… …………..
UHUSIANO NA MWANAFUNZI…………………………….
NAMBA ZA SIMU…………………………………………….

**<u>TAARIFA ZA MAENDELEO(REPORT FORM)YA KITAALUMA ZA MWANANGU</u>.CHAGUA KWENYE ORODHA ILIYOPO HAPO JUU 1-4**

ZITUMWE KWA JINA………………………………………AMBAE NI……………………AU…………………………AMBAE NI…………………………………………….
NAMBA YAKE YA SIMU YA WHATSAPP…………………../…………………….AU
Email…………………………………………

MUHIMU;

TAFADHALI UNAPOHITAJI KUPATA TAARIFA SAHIHI ZA SHULE WASILIANA NA NAMBA ZIFUATAZO.

1. MKUU WA SHULE (0658819057)
2. MAKAMO MKUU WA SHULE (0657240611)
3. MWANDAMIZI MALEZI (0689499869)


**DIFFERENT KWEMARAMBA SECONDARY SCHOOL UNIFORMS.**





1. Shirt, trouser , black tie and the pair of shoes





2. Black and white pull neck sweaters and the damu ya mzee(maroon) shamba dress.



. Dark blue track suit ya michezo na Boshori la rangi ya bendera ya taifa



**White long sleeve shirt, long black skirt, white and maroon hijab, and maroon shamba dress**